


# NDIPO YESU AKAJA

 ...na kwa Jina kuu la Mtoto Wako aliyetiwa mafuta, Bwana Yesu Kristo. Tunakushukuru kwa ajili ya Uzima Wake, na kwa ajili ya neema Yake ambayo imemwagwa ndani ya mioyo yetu, kwa Roho Mtakatifu.

<sup>2</sup> Kama tungesimama tu, kuhesabu baraka nyingi ambazo tumepewa, zitakuwa hazihesabiki. Tunashukuru kwa afya zetu, na kwa baraka zote kubwa ambazo pesa hazingeweza kununua. Umetujalia hizo kwa wingi, kwa neema Yako. Nasi ni watu wenye upendeleo kukujua Wewe.

<sup>3</sup> Na ni shauku ya mioyo yetu kwamba wale wasiokujua, na wasio na urafiki na Wewe, kwamba wafahamiane na Wewe, na dhambi zao zisamehewe, na kufanya urafiki Nawe, Baba. Kwa maana ulisema, “Mimi ni mpole na mnyenyekevu. Na msalaba ulikuwa rahisi na mizigo ilikuwa myepesi.” Nasi tunaomba tu ya kwamba utadhihirisha hilo kwa kila mmoja usiku wa leo. Kukitokea kuwa na wengine hapa wasiokujua, hebu na waje usiku wa leo na kukupokea Wewe. Wasaidie Wakristo wanapoendelea. Bariki nyimbo hizi, usiku wa leo, kutoka kwa wa—watu wanaoimba.

<sup>4</sup> Na utusaidie katika uamsho ujao. Siku hizi tano usiku, Bwana, tunaona hayo kuwa ni mapenzi Yako, tupate kuweka wakfu usiku huu kwa ajili ya ibada, kabla tu hatujasherehekea ufufuo mkuu; na kusulubiwa, kufufuka kwa Bwana wetu.

<sup>5</sup> Kuwa nasi sasa. Njoo kwenye Neno Lako, Bwana, na utuhudumie, na jalia tuwe na ushirika katika Neno, kwa Roho wa Mungu. Katika Jina la Kristo tunaomba. Amina.

<sup>6</sup> Ni majaliwa makuu kujaribu kusimama mbele ya mtu mmoja, kuzungumza juu ya Bwana Yesu. Na nimeona, katika huduma yangu, haijalishi kwa Mungu, kama kuna dazeni moja, au kuna maelfu. Yeye ana Ujumbe ule ule wakati wote kwa ajili ya watu, ambao ni neema Yake.

<sup>7</sup> Somo letu usiku wa leo, linaanza nyuma pamoja na mojawapo ya mandhari nzuri sana ya Maandiko. Nafikiri ya kwamba Maandiko yote ni makamilifu tu. Hakuna kosa linaloweza kupatikana kwa Neno la Mungu. Ni kamilifu tu. Lakini, andiko ambalo tunalizingatia, ni mojawapo ya mafungu mashuhuri ya Maandiko. Ni moja ya mihuri ya Umasihi Wake.

<sup>8</sup> Mnajua, watu wanaweza kuja hapa duniani, na wanaweza kutoa kauli za kila aina na ahadi za kila namna, lakini iwapo hawawezi kutimiza ahadi hizo, mbona, ahadi zao hazifai sana. Lakini mtu anapokuja na anaweza kutoa ahadi, na kisha

anaweza kutimiza ahadi hiyo, hilo hulifanya neno lake liwe la kutegemewa.

<sup>9</sup> Naye alikuwa ndiye Mwanadamu pekee aliyepata kuishi duniani, anayeweza kutoa tamshi hili, “Ninao uwezo wa kuutoa uhai Wangu, na ninao uwezo wa kuutwaa tena.”

<sup>10</sup> Nimejaliwa katika huduma yangu, kusimama kando ya kaburi la waanzilishi wengi mashuhuri wa dini, waanzilishi mashuhuri kama vile Muhammad na nyingi za dini nyingine nyingi mashuhuri za ulimwengu. Lakini kila moja yazo ina mahali palipotiwa alama ambapo mwanzilishi wao alifia, na kuzikwa, na amelazwa pale mpaka wa leo.

<sup>11</sup> Na bado, katika hali ya asili, kamwe sijapata fursa ya kusimama karibu na kaburi lile lililo wazi ambapo Kristo alilazwa, wala kaburi lisingeweza kumshikilia. Kwa maana Yeye Ndiye aliyesema, “Ninautoa uhai Wangu; hakuna mtu anayeundoa Kwangu. Ninauweka chini na ninautwaa tena.”

<sup>12</sup> Na ndiyo dini pekee ulimwenguni inayoweza kuthibitishwa kuwa ya kweli, ni dini ya Kikristo. Bwana wetu, sio tu kwamba aliwafia watu Wake, bali alifufuka tena kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwao. Naye amepaa Juu, usiku wa leo, na ameketi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu. Naye Roho Wake anaishi katika Kanisa Lake, pamoja na watu Wake, akifanya mambo yale yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani; akiendeleza huduma Yake.

<sup>13</sup> Na baada ya asubuhi hii, Roho Mtakatifu akishuka kwa uzuri sana na kutuogeha katika uzuri Wake mkuu, nilivuviwa tu kunena maneno hayo na kusema, kwamba, siku moja tukufu kwamba karama zote zilizoko kanisani zitawekwa tu kando, juu ya meko, tuseme. Naye Roho Mtakatifu, Mwenyewe, atachukua tu mamlaka juu ya Kanisa, kwa upendo wa Kiungu, hata wagonjwa wataponywa, vipofu wataona, viwete watatembea, bila kuwekewa mikono. Itakuwa tu ni mwungano mmoja mkuu.

<sup>14</sup> Basi tuliposimama asubuhi ya leo, katika wakati na majira tuliyomo, na kumwona mtu huyo akitembea. . . au akiwa amewekwa hapa huku ameinamisha kichwa chake katikati ya magoti yake, akiwa na ugonjwa wa uti wa mgongo uliokuwa umemwinamisha namna hii, na kumkunja. Na akiwa ameketi pale, alianza kuyumba-yumba huku na huko, kule nyuma.

<sup>15</sup> Kisha kumuona mtu huyo akirudi na kuketi chini, baada ya kupitia mstari wa maombi, na kujua kwamba alikuwa ametoa lile tamshi, na kusema, kwa miaka mingi, alikuwa hawezi kusikia vizuri sana masikioni mwake, ndipo kumwona Bwana Yesu akifungua masikio hayo kikamilifu sana, hata aliweza kusikia mnong’ono mdogo sana. Akarudi na kuketi chini na kuweka mikono yake juu ya masikio yake na kulia. Mfanyabiashara; mtu ambaye alikuwa ameendesha gari mamia ya maili kufika hapa.

<sup>16</sup> Ndipo, baada ya hayo, jukwaani, shuhuda za hao watoto wakija hapa, watu ambao walikuwa katika hali mbaya, ya kila aina ya magonjwa, kutoka kote nchini, wakitoa ushuhuda wa hali zao, na jinsi walivyokuwa wakifa kwa kansa na mambo mbalimbali. Nao hawa hapa, wazima, wameponywa. Hilo ni moja tu ya mathibitisho ya Umasihi Wake unaoendelea.

<sup>17</sup> Ni thibitisho kwamba Ukristo ni wa Kweli. Hakuna dini nyingine iliyo ya Kweli ila Ukristo. Na ni Kweli. Kristo ndiye Kweli. Naye...Dini ya Kristo haikufa pamoja na Kristo. Huenda ilikufa pamoja Naye, bali ilifufuka pamoja Naye, pia. Naye, usiku wa leo, angali anathibitisha Umasihi Wake mkuu.

<sup>18</sup> Tunafundishwa, katika kitabu fulani kidogo nilichokuwa nikisoma siku moja, kiitwacho, *Mfalme wa Nyumba ya Daudi*. Ninaamini kiliandikwa na mtu anayeitwa Ingraham. Na inasemekana kuwa, sehemu yake, ni kweli, na imetolewa kwenye hati fulani za kale, kutoka kwenye maandishi ya ngozi kutoka miaka mingi, mingi huko nyuma. Kwamba, kulikuweco na kijana Myahudi, kule Palestina, wakati ule ule Yesu alipokuwa kule. Naye, akimwandikia baba yake huko Alexandria, alikuwa akiwasiliana sana na baba yake, kuhusu Yohana Mbatizaji na Yesu aliyejitua Mwenyewe "Masihi." Na hapo ndani anatoa picha nzuri ya mandhari yetu usiku wa leo.

<sup>19</sup> Alisema kwamba Martha na Mariamu na Lazaro walikuwa marafiki wa karibu wa Yesu. Kwamba, baada ya kifo cha Yusufu, kwamba walikwenda... Alikuwa kuishi pamoja nao, na kuwa pamoja nao. Lazaro alikuwa akijifunza kuwa mwandishi hekaluni. Nao Martha na Mariamu pia walikuwa... Hawakuwa na baba wala mama. Kwa hiyo, walitengeneza mapazia kwa ajili ya hekalu, vitambaa vidogo na kadhalika, kazi ya ufumaji, na hiyo ikawapa kitu cha kufanya. Naye Yesu akaja kuishi pamoja nao, kabla hajajitambulisha Mwenyewe ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi.

<sup>20</sup> Naye Lazaro alikuwa ameshuka kwenda mtoni, kusikia mahubiri ya Yohana. Kwa hiyo akarudi na kuwaambia ni nabii mkuu jinsi gani aliyekuwa ametoka Galilaya, huko nyikani, na kile alichokuwa akitangaza, kwamba kuja kwa Masihi kulikuwa kumekaribia. Naye Lazaro hakujua ya kwamba Yule hasa aliyekuwa akizungumza naye alikuwa ndiye Masihi, Mwenyewe.

<sup>21</sup> Basi siku moja alimshawishi Yesu, tuseme, ashuke pamoja naye, wakamsikilize nabii huyu akihubiri. Naye Yohana, kule chini, hajavikwa maneno makubwa ya ufasaha; mtu wa kawaida tu, asiyevaa kama kuhani mkuu.

<sup>22</sup> Kwa maana, Mungu hakai katika jinsi tunavyovaa. Mungu hajali sana juu yake, mradi tu tumevaa kwa heshima na kuonekana sawa. Sio lazima ukosi wako upinduliwe, au kuvaa kilemba kichwani mwako. Mungu anataka uwe na moyo mnyenyekevu na mtiifu. Huo ndio Mungu anaangalia.

23 Naye alipomwona Yesu akija pamoja na Yohana, kwenye ubatizo wake, Yohana aligeuka na kutazama, akasema, “Tazameni Mwana-kondoo wa Mungu aziondoaye dhambi za ulimwengu.”

24 Ndipo Yesu alipobatizwa na Yohana, wanasema kwamba alirudi baadaye kwenye nyumba ya Lazaro na Martha. Naye alipokuwa akiishi huko, akila mezani pao, akalala vitandani mwao huko Bethania. Basi siku moja, Mungu alizungumza na Yesu na kumwambia, “Nataka uondoke mahali hapa, uende mahali nitakapokuonyesha.”

25 Sasa, tunajua ya kwamba Biblia ilisema, katika Yohana Mtakatifu 5:19, Yesu alisema, “Sifanyi neno isipokuwa Baba anionyeshe kwanza la kufanya.”

26 Na sasa ilimbidi Mungu kumwonyesha Yeye, basi, la kufanya, la sivyo hangeliondoka Bethania. Kwa hiyo akatoka, kama safari ya siku moja, au mbili.

27 Na muda si muda, Lazaro akawa mgonjwa, nao wakatuma mtu kumwita Yesu. Lakini, badala ya kuja, Yesu alipuuza tu wito huo.

28 Sasa si ingekufanya ujisikie visivyo kawaida kama mchungaji angefanya hivyo? Ingekufanya ujisikie kama, “Naam, yeye hatujali.”

29 Lakini, loo, kama ungetulia tu kwa dakika moja, kukumbuka jambo hili, kwamba, “Mambo yote hufanya kazi kwa manufaa ya wale wanaompenda Mungu.” Hakuna kitu duniani kinachoweza kuharibika, mradi tu uko ndani ya Mungu. “Hatua za mwenye haki huongozwa na Bwana.”

30 Na kisha wakaagizia tena Yesu aitwe. Naye, inaonekana, akapuuza wito wao na kuenda zake tu. Baada ya siku nne kupita, akasema, “Rafiki yetu, Lazaro, amelala, na kwa ajili yenu ninafurahi kwamba sikuwapo.” Kwa maana, kama angalikuwa pale, wangukuwa wakijaribu kumfanya afanye jambo ambalo halikuwa mapenzi ya Mungu.

31 Loo, jinsi ningeweza kutulia hapa kwa muda! Jinsi ambavyo, mara nyingi, kwa nia njema, watu hujaribu kuwaita watu watoke katika mapenzi ya Mungu. Mtu anapaswa kujua wito wake kabisa. Unapaswa kujua unachofanya, na sio kwa njia ya kubahatisha tu, au kuruhusu pesa ikuvute kutoka sehemu moja hadi nyingine, au umaarufu kufanya hivyo. Haijalishi wewe ni maarufu kiasi gani, ni tajiri kiasi gani, sikuzote unapaswa kwanza kumtafuta Mungu, ili kujua mpango Wake na mapenzi Yake.

32 Sasa, wakati Lazaro alipokuwa mgonjwa, ilionekana ajabu kwamba Yeye hangerudi. Lakini Yesu akasema, “Ninafurahi sikuwapo.”

<sup>33</sup> Maana, wangukuwa wanamshawishi, kusema, “Sasa, kwa nini usije *huku*? Kwa nini usifanye *hivi*? Na kwa nini usimfufue? Uliwafufua wengine.” Lakini, Yesu alijua vizuri zaidi. Yesu alijua ni nini mapenzi ya Baba.

<sup>34</sup> Na, loo, ni majaliwa yaliyobarikiwa jinsi gani, kwamba tunaweza kujua mapenzi ya Baba. Ikiwa tutamtafuta Mungu, Mungu atafanya mapenzi Yake yajulikane.

<sup>35</sup> Ni afadhali nijue kwamba nilikuwa katika mapenzi ya Mungu, kama sikupata kusema na mtu mwingine, kuliko kuwahubiria watu elfu kumi kila usiku, nje ya mapenzi ya Mungu. Afadhali nijue mapenzi ya Mungu. Naamini ni Daudi aliyesema, “Afadhali niwe mkeka wa mlangoni,” kwenye. . . au kitu fulani, “katika nyumba ya Bwana wangu, kuliko kukaa katika hema pamoja na uovu.”

<sup>36</sup> Ni majaliwa ya jinsi gani, kupata mahali petu na kukaa hapo. Haidhuru ibilisi anatemesha jinsi gani, anachosema, na jinsi anavyodhihaki, kaa moja kwa moja katika mapenzi ya Mungu.

<sup>37</sup> Angalia, basi, wakati Yesu aliposema, “Sasa, a—amekufa.” Walidhani alikuwa analala. Akasema, “Amekufa. Na kwa ajili yenu, ninafurahi kuwa sikuwapo. Lakini naenda kumwamsha.” Loo, jamani! Haikuwa ati, “Nitaenda nione kama naweza; nitaenda nijaribu.” Lakini, “Nitaenda nimwamshe.” Kwa maana, Yeye alijua, Mungu alikuwa amemwonyesha kwa ono, ya kwamba Lazaro angetoka kwenye kaburi lile. Wala haikuwa kazi ya kubahatisha. Loo, kama Mungu angeninii. . .

<sup>38</sup> Wakati wowote ambapo Mungu anaonyesha ono la kile kitakachotokea, itakuwa hivyo hasa, kama ono hilo linatoka kwa Mungu. Haina budi iwe! Jinsi ningeweza kutulia hapa katika somo langu, na kunukuu tu, kwa saa nyingi, matukio ninayojua.

<sup>39</sup> Nimeenda kwenye matukio ambayo ningewazia, “Ee Mungu, hakika utalifanya,” kutoka tu na kujaribu tu kuipima imani yangu dhidi yake. Lakini mara nyingi haifanikiwi.

<sup>40</sup> Lakini Mungu anaponyesha ono, loo, jamani, halina budi kutukia. Haliwezi kushindwa. Na kwa sababu Yeye anafanya hivyo sasa, ni thibitisho lisiloweza kukosea kwamba Yeye angali ni Masihi, ya kwamba Umasihi Wake umetiwa muhuri kwa ishara na maajabu ya uthibitisho wa Neno Lake lililobarikiwa.

<sup>41</sup> Na kisha kuwazia, ya kwamba, Lazaro, wakati alipokuwa mgonjwa. Hakuna anayejua ugonjwa ni nini hadi uwe nao nyumbani kwako mwenyewe. Nami nina hakika ya kwamba kila mmoja wetu, usiku wa leo, anaweza kuwahurumia Martha na Mariamu. Jinsi mtafuta riziki wao pekee waliyekuwa naye, ndugu yao, alilala kitandani mgonjwa. Na labda madaktari walikuwa wamemkatia tamaa. Tunafundishwa kwamba alikufa na kuvuja damu mapafuni, pengine kifua kikuu. Ndipo akafa kwa ugonjwa huo. Na wakati alipokuwa mgonjwa sana, na

daktari alikuwa amemkatia tamaa, halafu Yesu akakosa kuja kwa rafiki Yake.

<sup>42</sup> Sasa, huo ulikuwa ni wakati wa giza. Je, unaweza kuwazia hao wasichana wawili warembo wakiagizia Yesu aitwe, Naye akakataa kuja? Baada ya kuondoka kanisani na kukana dini ya kale ya Othodoksi, na walikuwa wamejitenga wenyewe na washirika wengine wa ulimwengu; nao walikuwa wakiweka tumaini lao lote kwa Mtu huyu, Kristo, Ambaye waliamini kuwa ndiye Masihi, Kristo; na halafu akawaalbisha!

<sup>43</sup> Loo, sote tulipata matukio kama hayo. Nakumbuka nilipoongoka kwa mara ya kwanza, jinsi ambavyo watu wangu walifikiri nilikuwa nimerukwa na akili. Naam, walisema, “Ukishika dini ya aina hiyo, utakuwa katika hospitali ya wendawazimu katika siku chache.” Umekuwa na jambo lile lile, la watu kukudhihaki, na wenzako wakisema kwamba umerukwa na akili. Lakini maadamu imani yako iko katika Kristo, kila kitu kitatokea sawa. Kamwe usiwe na wasiwasi kuhusu hilo. Pia naweza kukumbuka jinsi ambavyo watu . . .

<sup>44</sup> Ngingekutana na rafiki yangu mvulana, na wasichana wadogo niliokuwa nikitembea nao, nikutane nao barabarani. Naye akasema, “Billy, umekuwa mtakatifu anayejifingirisha.” Sikujali, kwa maana nilijua kwamba kitu fulani kilikuwa kimetukia, kitu fulani kilitukia.

<sup>45</sup> Huku, moyoni mwangu, niliamini kuwa ni Roho Mtakatifu halisi, wa kweli. Miaka ishirini na minne imepita, na angali ametia nanga mle usiku wa leo. Nina azimio lile lile la kumtumikia, kama nilivyokuwa usiku wa kwanza nilipomwahidi, kwenye kibanda kile kidogo cha mbao. Bila shaka. Kitu fulani kimeshikilia! Saa za giza zimekuja. Misiba imekuja. Masikitiko yamekuja. Kifo kimekuja. Lakini, mbele ya hayo yote, ninaegemea kwenye tumaini hilo zuri ambalo Yeye alisema, “Mimi ndimi ufufuo na Uzima; yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi.”

Imani yangu haijajengwa juu ya kitu kingine  
Ila Damu ya Yesu na haki;  
Yote yanayoizunguka nafsi yangu yakitoweka,  
Basi Yeye ndiye tumaini na nanga yangu.

Juu ya Kristo, Mwamba imara, tunasimama;  
Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.  
(Bila shaka!)

<sup>46</sup> Loo, lazima ilikuwa ni wakati wa giza; wakati daktari wao alikuwa amewakosea, wakati rafiki yao alikuwa amewaacha, naye Lazaro sasa alikuwa anakufa. Ndipo siku ya nne ikafika, akavuja damu mara yake ya mwisho, akaenda kuwa pamoja na Mungu. Wakamtoa nje; wakatoa damu mwilini mwake, wakatia manukato na marashi katika mishipa yake, wakamfunga sanda

na kumlaza kaburini. Naye akalala pale, siku nne, amekufa. Mwili wake ulikuwa unanuka.

47 Sasa, mtu yeyote anajua kwamba mwili wa mwanadamu hutengana vipande vipande baada ya saa sabini na mbili.

48 Hiyo ndiyo sababu Yesu alipaswa kufufuka kabla zile siku tatu kwisha. Na saa sabini na mbili, uharibifu unaingia.

49 Naye Daudi, katika Biblia, alisema, miaka mia nane kabla ya Kristo kuzaliwa, chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu. Kasema, “Sitamwacha mtakatifu Wangu aone uharibifu, wala sitaiacha nafsi Yake kuzimu.”

50 Hiyo ndiyo sababu Yeye alisema, “Uharibuni mwili huu, Nami nitauinua katika siku tatu.” Alijua kwamba hakuna uharibifu ungeingia. Hiyo ndiyo sababu alikufa Ijumaa alasiri, kisha akafufuka tena Jumapili asubuhi, ni kwa sababu alijua uharibifu usingeweza kugusa hata seli moja ya huo mwili uliobarikiwa.

51 Kwa maana, Neno la Mungu halikosei kabisa. Loo, jamani! Yeye hulitimiza Neno Lake, kikamilifu. “Hatamwacha mtakatifu Wangu aone uharibifu, wala hataiacha nafsi Yake kuzimuni.” Neno la Mungu lisiloweza kukosea halingeweza kushindwa. Huo hapo mwili Wake umelala.

Hakika, watu wanauliza. Walisema, “Ati siku tatu mchana na usiku?”

52 Lakini, ilikuwa ndani ya siku tatu mchana na usiku, alisema. Alijua kwamba isingeweza kuwa siku tatu mchana na usiku kabisa, kwa sababu uharibifu ungeingia.

53 Kwa hiyo, huyu hapa Lazaro, siku nne zilikuwa zimepita. Pua ilikuwa tayari imeanguka ndani, usoni. Vidole vilikuwa vimegeuka tayari. Mabuu wa ngozi walikuwa wameanza kutambaa ndani ya mwili wake na kula nyama yake.

54 Loo, hapana shaka ilikuwa saa ya giza kuu kuliko zote familia hiyo ndogo iliyopata kuona! Rafiki yao ameondoka. Kanisa lao; walikuwa wametengwa. Ndugu yao alikuwa amekufa. Nao watu walikuwa wakiwadhihaki na kuwacheka, wakati maskini hao wasichana wawili wakiwa wameketi pamoja nyumbani, wakiwa wamevaa shela zao nyeusi usoni, kama ilivyo desturi ya watu wa mashariki. Wakiwa wameketi pale, wakilia na kuomboleza, kwa ajili ya kuondoka kwa ndugu yao. Hao hapo.

55 Hakuna mtu ila ambaye ameketi katika aina hizo za nyumba; hakuna mtu ila wale ambao wameketi kando ya wapendwa wao! Tunajua, wengi wenu mnajua, jinsi tunavyoketi karibu na mpendwa wetu. Roy, ninaweza kukuona umeketi kando ya mvulana huyo mdogo. Ndugu Roberson, ninaweza kukuona wewe na Dada Roberson mmeketi kando ya mama yake. Loo, jinsi ambavyo wengi wenu! Ninaweza kujiona nimeketi kando

ya mtoto wangu mdogo, aliyefariki, wa karibu umri wa miezi minane. Tunajua mambo hayo ni nini. Loo, ni saa zenye giza jinsi gani!

<sup>56</sup> Lakini ilikuwa saa ya giza zaidi ambayo familia hiyo ndogo ilikuwa imeona. Na yapata wakati huo, Yesu akaja jukwaani. Ni, kwa kawaida, hivyo ndivyo anavyofanya. Ni katika saa yenye giza mno, na ndipo Yesu anajitokeza jukwaani.

<sup>57</sup> Ilikuwa huko chini sana Babeli, asubuhi moja, miaka mingi iliyopita. Wakati watoto watatu wa Kiebrania, waliokuwa wamechukuliwa kule chini, mateka, mbali na nchi ya uenyeji wao. Walikuwa na huzuni kwa sababu walikuwa mateka. Walikuwa na huzuni kwa sababu hapakuwa na mahali pa kuabudia. Lakini bado waliishi waaminifu kwa Mungu. Ndipo likaja kundi la wadanganyifu, nao wakatoa tangazo, kwamba, “Yeyote ambaye hataisujudia sanamu,” ambayo ilikuwa kinyume na dini yao, “angetupwa katika tanuru ya moto.” Ndipo mfalme, pamoja na ugomvi wake mkuu, akajitokeza na kusema, “Yeyote ambaye hataisujudia sanamu hii, lazima aingie katika tanuru hii ya moto na kuteketezwa.” Sasa, kulikuwa na wakati wa majaribu.

<sup>58</sup> Na daima kuna wakati wa majaribu. “Kila mwana amjiaye Mungu, haba budi kujaribiwa kwanza.” Loo, ninakupenda. Loo, sikuitishi, lakini, baada ya kupita, hutoa matunda mazuri ya upole. Wakati wa majaribu, wakati moto ukiwa mkali! Jinsi kila Mkristo, katika nyakati mbali mbali, alipitia wakati huo wa kujaribiwa. Nayo Biblia ilisema, “Kama hatuwezi kustahimili majaribu hayo, tunakuwa watoto haramu, na si watoto wa Mungu.” Kwa hiyo, mtoto halisi katika wakati wa kujaribiwa, ambapo huu ulikuwa, hawatembezi kwa kuona. Macho yao ya kimwili yamefungwa kwa vitu vilivyo karibu nao. Wanaenenda tu kwa imani ya Bwana Yesu Kristo, wakilitazama Neno Lake, na kuamini ya kwamba atatimiza kila Neno jinsi hasa alivyosema angelitimiza. Wakati wa majaribu, majaribio!

<sup>59</sup> Nasi tunaona, wakati huu wa kujaribiwa ulipowajia hawa watoto watatu wa Kiebrania, walithibitika kuwa waaminifu. Walisema, “Hatutaisujudia hiyo sanamu.” Loo, jamani!

<sup>60</sup> Ndipo, lile tangazo kuu lililokuwa limetiwa sahihi, walienda na kuwakusanya pamoja, wakavuta mikono yao nyuma yao, wakawapitisha juu ya ubao mkubwa, njia ya kupitia, kutumbukia kwenye tanuru iliyokuwa imefanya anga kuwa jekundu kweli, joto mara saba kuliko ilivyowahi kuwashwa. Basi walipokuwa wakipanda juu ya ubao huu, wakijua ya kwamba mioyoni mwao, hawakuona jinsi ambavyo Mungu angefanya jambo hilo. Lakini walijua ya kwamba Mungu angeweza kufanya hivyo. Yalikuwa ni majaliwa yao kutembea hadi kufa kwao, tuseme, kulitimiza Neno la Mungu.



61 Ndipo walipokuwa wakienda kule, labda ilikuwa ndiyo saa ya giza kuliko zote waliyopata kuona. Hawakuwa na—na nyumba ya kwenda, katika dunia hii. Walikuwa mateka. Walikuwa tu kama watumwa. Walikuwa wameletwa kutoka katika nchi ya uenyeji wao. Hawakuruhusiwa kwenda kwenye ibada ya umma. Waliabudu sanamu katika nchi hiyo; kwa hivyo hawakuweza kwenda kwenye ibada ya sanamu, wala hawangeweza kuwa na majaliwa ya nchi ya uenyeji wao. Walikuwa mateka. Lakini, jambo moja, huwezi kumfunga mwaminio kutoka kwa Mungu wake. Hapana, huwezi.

62 Ndipo asubuhi hiyo, walipokuwa wakienda kule, wakijua ya kwamba walisimama peke yao pamoja na Mungu. Ndipo walipoanza kupiga hatua zao, walipokuwa wakipanda juu, labda, ile saa yenye giza mno waliyopata kufikia. Ndipo joto la tanuru likaanza kumulika usoni mwao. Ndipo walipopiga hatua yao ya mwisho ya kuuaga ulimwengu huu, wakaingia kwenye tanuru hiyo ya moto, ndipo Yesu akaja wakati huo. Naye akashuka katika tanuru hiyo ya moto, akichomoa mtende kutoka kwenye miti isiyokauka kutoka Mbinguni, ndipo akaupeperusha moto kutoka kwao.

63 Mpaka, baada ya kuungua, labda kwa saa moja au zaidi, mfalme alichoka na kusema, “Fungueni, na tuone kilichotendeka.”

64 Basi waliposhusha kile kifuniko kikubwa cha tanuru, na kile kifuniko kikubwa cha chuma au cha shaba kikaanguka chini, mfalme akachungulia ndani. Naye akasema, “Kwani tuliweka wangapi humo?”

Akasema, “Tuliweka watatu.”

65 Akasema, “Kuna wanne mle. Na Mmoja wao anaonekana kama Mwana wa Mungu.”

66 Inaweza kuwa giza, nyakati za joto, zinaweza kuja nyakati za majaribu, lakini Yesu daima yuko jukwaani ikiwa tu tutakuwa wakweli na waaminifu.

67 Ilikuwa ni maskini mwanamke mmoja wakati mmoja, ambaye alikuwa ametumia pesa zake zote, kwa madaktari. Naye alikuwa ameuza shamba, na mifugo, labda. Na vyote alivyokuwa navyo alikuwa ameviuza; na kuwapa madaktari, kujaribu kuponywa. Hakuna hata mmoja wao ambaye angeweza kumsaidia. Basi alipokuwa ameketi peke yake, maskini mwili wake ulikuwa dhaifu, kwa sababu alikuwa akipoteza damu kwa miaka mingi. Wala hakuna kitu kingeweza kuonekana kumsaidia. Na hapo . . .

68 Alikuwa amesikia. Mwajua, “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno.” Alisikia kwamba huko mbali ng’ambo ya Galilaya, kulikuwa na Nabii kule, ambaye alikuwa akiwaponya wagonjwa. Lakini, hakuwa na pesa za kuvuka ziwa. Hangeweza kupiga makasia mashua, yeye mwenyewe; alikuwa dhaifu sana.

Wala hangeweza kuwa na pesa za kumlipa mtu mwingine, kwa sababu alikuwa ametumia zote alizokuwa nazo, kwa ajili ya madaktari, na bado alikuwa hawezi tu kama alivyowahi kuwa.

<sup>69</sup> Asubuhi moja, akiwa ameketi nje, vile tungewazia, ukumbini, huku maskini vidole vyake vikitetemeka, akijaribu kufanya ufumaji kidogo ama kushona. Alipotazama kule chini, kulikuwa na kelele kidogo ikitokea huko chini kando ya bahari. Ndipo mashua ndogo ikasukumwa kwenye mierebi, ikatokea alitazama. Na baada ya . . .

<sup>70</sup> Alikuwa ameketi hapo, akiwazia, “Sasa pesa zangu zote zimekwisha. Nitafanya nini tena? Tumepata . . . pengine nitafukuzwa nyumbani. Rehani tayari imechukua hizo. Hatuna hata chakula, wala hakuna kingine. Wala siwezi kupata faraja.” Pengine ilikuwa ndiyo saa yenye giza zaidi aliyowahi kuona.

<sup>71</sup> Ndipo yapata wakati huo, ile mashua ndogo ikaingia ndani, naye Yesu akaja. Anashuka hadi mtoni, huku maskini mwili wake ukitetemeka.

<sup>72</sup> Na kumbukeni tu, kwa sababu Yesu amekuja, kila ibilisi katika kuzimu atajaribu kukuzuia usimkaribie. Hiyo ni kweli. Huenda ukasikia Ujumbe, lakini ibilisi ataketi moja kwa moja begani mwako, na kusema, “Usisikilize. Usisikilize. Usisikilize.” Lakini usimwamini.

<sup>73</sup> Alisema, “Yeyote atakaye, anaweza kuja na kunywa maji ya Uzima, bure.”

Usisikilize, kwa maana yeye ni ibilisi.

<sup>74</sup> Ndipo maskini yule mwanamke akashuka mpaka pale Yesu alipokuwa anakuja, nao watu wakimzunguka, maskini, na kadhalika.

<sup>75</sup> Na hapo alisimama kuhani na viongozi wo—wote wakuu wa dini yake. Nao walikuwa wakimdhihaki, na kusema, “Ei, ati Wewe Ndiwe unayewaponya wagonjwa, sivyo? Vema, tuna wagonjwa wengi sana. Hebu tukuone ukiwaponya. Vema, Wewe Ndiwe unayewafufua wafu ati, sivyo? Tuna makaburi yaliyojaa hapa. Hebu tukuone ukiwafufua.”

<sup>76</sup> Hakuwajali hata kidogo. Akaendelea tu. Alikuwa na jambo moja la kufanya, hilo lilikuwa ndilo jambo ambalo Mungu alimwonyesha kufanya. Hakuna pungufu wala cha zaidi!

<sup>77</sup> Mkristo anapofikia mahali hapo, ambapo atajiweka kando wala asisikilize kashfa zote na upuuzi ambao unasemwa, na yote yanayoendelea; na kuwa na nia moja, hiyo ni kufanya mapenzi ya Mungu, ambayo Mungu alikutuma kufanya, kutakuwa na siku tofauti na kanisa tofauti.

<sup>78</sup> Huyu hapa anashuka kwenye umati huu. Naye Yesu alikuwa akitembea, katika mwendo Wake wa polepole, taratibu.

<sup>79</sup> Nao watu walikuwa wakimkimbilia, wakisema, “Ati Wewe ndiwe yule Nabii? Je, Wewe ni *hiki*? Wewe ni *kile*? Aisee, vipi kuhusu kuja hapa na kunifanyia kitu? Hebu nikuone ukifanya mwujiza. Tungependa kukuona ukigeuza maji kuwa divai; hii hapa jagi iliyojaa maji. Ningependa kuonja kidogo. Wanasema ilikuwa divai nzuri. Fanya *haya* kuwa divai. Hebu nisikie ladha yake.”

<sup>80</sup> Hakuinua hata kichwa Chake. Aliendelea tu mbele. Hilo linanifanya nimpende.

<sup>81</sup> Unajua, inahitaji maskini watu duni kugombana na kubishana. Mtu mkubwa kamwe hajali kitu kama hicho. Wakristo hawatambui kile ambacho ulimwengu unasema, ikiwa wanataka kusema chochote wanachotaka. Wamepata . . . Wao ni wakubwa sana kuona vitu hivyo vidogo. Wanaendelea tu mbele, kuendelea tu.

<sup>82</sup> Maskini huyo mwanamke akawazia, “Sasa, ndiyo saa pekee ambayo nitawahi kumwona; nafasi yangu ya mwisho. Fursa pekee ambayo nimewahi kupata. Nami kwa kweli ninaamini, kama ningeweza tu kugusa vazi la Mtu huyo, ningeponywa.” Ni imani ya jinsi gani! Ni wakati wa jinsi gani!

<sup>83</sup> Na, hapa, umati unapojaribu kumzuia, anapiga magoti, kwa njia fulani, na kutambaa katikati ya umati huo wote, mpaka akagusa vazi Lake. Naye akarudi nyuma na kusimama kwenye umati wa watu.

Yesu akageuka na kusema, “Ni nani aliyenigusa?”

<sup>84</sup> Mbona, umati ukasema, “Mbona, hakuna aliyekugusa.” Kila mtu akakana.

<sup>85</sup> Naye Petro akamkemea. Akasema, “Bwana, kila mtu amekuwa akikupitia.”

Akasema, “Lakini ninaona kwamba nguvu zimenitoka.”

<sup>86</sup> Naye akatazama pande zote mpaka akampata. Naye akasema, “Imani yako imekuokoa.”

<sup>87</sup> Saa yake ya giza kuliko zote. Nayo Biblia ilisema, ya kwamba, “Alijisikia ndani yake, kwamba aibu . . . kutokwa na damu kumekoma.”

<sup>88</sup> Je, Bwana Yesu yeye yule hakuwa hapa asubuhi ya leo? Kwa mtu anayeketi pale, aliye na kansa iliyoenea sana, mpaka yeye . . . Daktari alisema, “Anaweza kuishi kwa muda kidogo tu.” Na alipokuwa akipita kando ya madhabahu, katika saa yenye giza kuliko zote aliyopata kuona, ndipo dakika kumi na tano akasimama kule nyuma. Na ilibidi aje hapa na kusema, “Hisia zote nzito zimenitoka.” Saa yenye giza kuliko zote, ndipo Yesu akaja.

<sup>89</sup> Ndugu Burns anayeketi pale, wakati . . . Maskini mwenzake mpendwa aliye Utukufuni, usiku wa leo. Jinsi ilivyokuwa,

alikuwa amelala kule, kwenye hospitali hapa Louisville, akiwa na kansa kwenye wengu. Nao madaktari walikuwa wakimkatia tamaa. Na mimi na Ndugu Wood tulikuwa nje m—msituni, tukiwinda kuchakulo. Nasi tukaingia, ndipo kitu fulani kikanisukuma kwenda Louisville. Kwa nini? Sijui.

<sup>90</sup> Nami nikasema, “Ndugu Wood, endesha gari moja kwa moja mpaka pale pembeni, ninaenda Sutcliff. Ndipo ukirudi huku, unaweza kunichukua.” Nilisubiri na kusubiri. Singeweza kumwona popote. Ndipo baada ya muda kidogo, nikamwona akipiga kona hiyo nyingine, na kupita barabarani, akiwazia kwamba Sutcliff ulikuwa ni mtaa mwingine juu. Kama mtu huyo angeangalia tu, angeona Sutcliff haukuwepo. Naye anashughulika na Sutcliff. Anajua mahali ilipo.

<sup>91</sup> Lakini maskini Dada Burns, anayepumzika pamoja na Mungu, usiku wa leo, alikuwa amesimama nyumbani kwake; akachukua picha hiyo ndogo yenye Malaika wa Bwana juu yake, akapiga magoti mbele yake na kusema, “Ee Mungu, nisaidie kumtafuta Ndugu Branham kwa ajili ya mume wangu mpendwa.”

<sup>92</sup> Ndipo anaenda katikati ya mji kulipa bili ya umeme, bila kujua nilikokuwa katika ulimwengu huu mpana. Ndipo akaja. Nilisubiri kwa zaidi ya nusu saa. Nami nikaendelea kuona gari likipitia kona hiyo nyingine. Nikasema, “Amepotea. Lazima nipande kule.” Ndipo nilipofika tu kwenye kona, naye akapiga kona, nipate kuingia kwenye gari, na yapata wakati huo, Dada Burns akafika hapo kwenye kona.

<sup>93</sup> Na hapo, kwa maombi ya imani, Mungu akamponya mumewe. Naye yule pale ameketi usiku wa leo. Ilikuwa katika saa yenye giza kuliko zote, ndipo Yesu akaja.

<sup>94</sup> Tunafikiri tu kwamba tumepotea na tumeachwa. Nawe unapoanza kujisikia...Endelea tu kushikilia. Atakuwepo. Usichoke.

<sup>95</sup> Ilikuwa ni saa ya giza zaidi ambayo maskini Georgie Carter alikuwa amewahi kuona, kule chini Milltown. Alikuwa mfuasi wa kanisa ambalo halikuamini katika uponyaji wa Kiungu. Walidhihaki na kuufanyia mzaha uponyaji wa Kiungu. Na hapo maskini mwanamke huyo amelala katika hali hiyo. Ndipo Bwana akanena nami hapa chini kitandani, na kusema, “Shuka uende Milltown.” Sikuwa nimesikia kuhusu mahali hapo.

<sup>96</sup> Nikaja kwenye jukwaa lili hili, nami nikasema, “Bwana amenituma mahali paitwapo Milltown. Kuna maskini mwana-kondoo ambaye amenaswa kwenye vichaka, naye analia apate usaidizi.” Hakuna aliyejua ni wapi.

<sup>97</sup> Ndipo Ndugu George Wright, alikuwa hapa asubuhi ya leo, akasema, “Najua ni wapi. Iko chini tu ya kwangu.” Nilishuka Jumamosi iliyofuata. Nikatazama kila mahali, kisha nikaanzisha mkutano katika kanisa la kale la Baptisti.

<sup>98</sup> Ndipo Bw. Hall akaniongoza kule kumwombea msichana huyu mdogo, nami nikamwombea. Watu wake waliondoka nyumbani. Hawakutaka kujihusisha nalo, kwa maana kanisa lao lilikuwa limewaambia, “Watu wowote,” waliohudhuria mkutano wangu, “watatengwa na kanisa.” Hapo alikuwa amelala, miaka tisa na miezi minane, amelala chali, asiweze hata kusogea. Alikuwa amelia. Alikuwa ameomba. Mpaka, unaweza kwenda, mpaka siku hii, na kuangalia. Kitanda chake kidogo cha bango, alikuwa amefuta ra—rangi yote nyuma yake, akimlilia Mungu, afanye jambo. Na hata hivyo, kanisa lake baridi na rasmi halikuamini katika uponyaji wa Kiungu na lingemkataza mtu yeyote kuja kumwombea kwa njia hiyo.

<sup>99</sup> Huko baba yake alikuwa shemasi, ama chochote kile, kanisani. Mama yake na hao wengine, nguzo kuu kanisani. Na hapo walikataliwa; matumaini yote yamekwisha. Madaktari walimkatia tamaa, miaka mitano hapo kabla. Alikuwa na uzito wa takriban pauni thelathini na saba tu; hamna kitu ila mifupa. Maskini miguu yake midogo ilionekana kama mipini ya fagio. Na hapo alilala bila kitu ila ngozi tu juu ya mfupa.

<sup>100</sup> Siku moja, nikishuka kwenda huko... Naye mama yake akatoroka; baba yake akaondoka nyumbani. Hawakuwa na uhusiano wowote na mlokole huyo. Basi siku moja, niliingia ndani nipate kumwombea, Nikasema, “Ewe msichana mdogo, hivi uko tayari kuinuka na kubatizwa katika Jina la Bwana Yesu, kuziosha dhambi zako, na kumtumikia?”

<sup>101</sup> Ilibidi nisogee karibu nisikie alichosema. Akasema, “Nitafanya chochote.” Nikaangalia, juu ya ninii yangu... kitanda chake, na hapo mlikaa kitabu changu kidogo, kinachoitwa *Yesu Yeye Yule Jana, Leo, Na Hata Milele*. Nikamwombea, ilionekana kana kwamba haikusaidia chochote.

<sup>102</sup> Majuma mawili nikafanya mkutano. Nikaenda kubatiza kule Totten Ford. Basi siku hiyo mkutano ulikuwa unaisha, usiku huo. Ndipo wakati nikibatiza... .

<sup>103</sup> Kulikuwa na mhudumu mwingine kule juu ambaye alidhihaki na kufanyia mzaha mawazo yenyewe ya ubatizo wa maji, na kutumia Jina la Bwana Yesu Kristo. Alisema, “Kama yeyote wa watu wangu anayeketi chini ya hema hii, alipata kumkaribia huyo mtu, ondoka hapa sasa. Sitaki uhusiano wowote nao.” Ndipo ikatokea Bw. Wright alikuwa ameketi pale, naye akasimama moja kwa moja na kutoka nje. Ndipo Jumapili iliyofuata... Sikuwahi kufungua kinywa changu na kusema neno juu ya mtu huyo.

<sup>104</sup> Nami nikapanda kule, mahali pa kuninii... .kubatizia kule juu kwenye Totten Ford. Ndipo nilipoingia majini, hao hapo watu kutoka kwenye uamsho wake, wamesimama ukingoni, kunifanyia mzaha nikibatiza katika Jina la Bwana Yesu. Ndipo nilipotoka ndani ya maji, yapata wakati huo Yesu akaja.

<sup>105</sup> Hili hapa kusanyiko lake lote linakuja, wakiwa wamevaa nguo zao nzuri, wakitembea kuingia kwenye maji hayo yenye matope, wakipiga mayowe, “Mungu unirehemu!” Nami nikabatiza kila mmoja wao katika Jina la Yesu Kristo, papo hapo kwenye shimo lile la maji.

<sup>106</sup> Tukaenda hadi kwa Ndugu George. Naye Ndugu George akasema, “Ndugu Branham, njoo kwenye chakula cha jioni katika dakika chache.”

<sup>107</sup> Nikasema, “Sharti niombe.” Nikaenda msituni, wala sikuweza kuomba, hapa na pale. Ndipo ghafla, giza lilipokuwa karibu kuingia, nikatazama, na kulikuwa na Nuru ikiangaza chini kwenye mti-mbwa mdogo, nayo ikasema, “Simama kwa miguu yako, kwa miguu yako, na uende kwa njia ya Carter.”

<sup>108</sup> Maskini mtoto Georgie amelala pale, akilia, na kusema, “Loo, mama, nitaachwa. Ataondoka leo, wala sitaweza kumwona tena.” Na hiyo ilikuwa ibada ya kumaliza, usiku huo, ya uamsho huo mkuu. Huyo hapo, huku matumaini yote yamekwisha, ilivyoonekana. Ndipo yapata wakati huo, Yesu akaja.

<sup>109</sup> Naye maskini mwanamke huyo amelala pale, uzito wake ulikuwa pauni thelathini na kitu tu. Nilipoingia pale na kumwekea mkono, nilisema, “Dada, Bwana Yesu alinitokea muda mfupi uliopita, kando ya kilima pale. Akasema nije hapa na kukuwekea mikono yangu, upate kuponywa.”

<sup>110</sup> Maskini mwili huo mdogo uliokonda sana ambao haujainuka kutoka kitandani kwa miaka tisa na miezi minane. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . alisimama kwa miguu yake na kukimbia kwenye piano, na kuanza kucheza:

Yesu, unihifadhi karibu na msalaba,  
Hapo pana Chemichemi ya thamani,  
Bure kwa wote, kijito cha uponyaji  
Kinachotiririka kutoka mlima wa Kalvari.

<sup>111</sup> Ilikuwa ni saa yenye giza kuliko zote ambayo Georgie aliwahi kuona, ndipo Yesu akaja.

<sup>112</sup> Mbunge Willie D. Upshaw, miaka sitini na sita kwenye kiti cha magurudumu, aliyesukumwa kutoka ukumbi wa bunge, hadi mahali mahali. Alikuwa ameombewa, mara mia kadhaa. Alikuwa makamu wa rais wa Shirika la Wabaptisti wa kusini, Wabaptisti wa Kusini. Mtu mashuhuri, mtu mzuri sana, mtu ambaye angekuwa Rais nchini Marekani, mwaka wa 1926, kama angeuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Lakini, alichukia wiski. Basi akagombea kwa tikiti ya kupiga pombe marufuku, wakati chama cha Democrat kingemchagua. Walisema wangemchagua, nao wangemchagua. Bila shaka, angeweza kushinda kwa urahisi. Alipendwa sana.

113 Lakini akasema, “Nisingebadilisha haki yangu ya mzaliwa wa kwanza, nipate kuwa Rais wa ulimwengu.” Haleluya! Mungu na atupe watu wa aina hiyo, katika Ikulu yetu hapa. Naam, bwana. Angewezaje kulala basi kama kiwete? Mgongo wake ulivunjika, tangu alipokuwa na umri wa miaka kumi na saba, naye alikuwa na themanini na sita.

114 Basi usiku mmoja, kule, mbele ya makumi ya maelfu ya watu, wakati Roy Davis alipomtuma huko. Naye akamleta ndani katika kiti cha magurudumu, baada ya Roy kumwombea, na mamia ya wengine. Wala kamwe sikusikia habari za huyo mtu maishani mwangu. Huyo hapo, ameketi kule nyuma, katika mkutano mwingine tu. Nikaenda jukwaani. Na yapata wakati huo, niliangalia, nami nikaona lundo la nyasi kavu, na mvulana mdogo akicheza. Roho Mtakatifu alipoanza kufunua, alimtaja na kumwambia kwamba alikuwa mbunge, na kwamba Yesu Kristo alikuwa amemponya.

115 Hapo, yeye, asiyejiweza, miaka sitini na sita kwenye kiti cha magurudumu, umri wa miaka themanini na sita, saa yenye giza kuliko zote aliyowahi kuona. Matumaini yote yalitoweka, kwa ajili ya uponyaji wake. Ndipo Yesu akaja. Naye mtu, aliyekuwa kwenye kiti cha magurudumu kwa miaka sitini na sita, akainuka na kukimbia jukwaani, akiwa na umri wa miaka themanini na sita, na kuigusa miguu yake, na kuruka-ruka juu chini. Ndipo akasimama katika mkutano wa Billy Graham na kuimba *Ninaegemea Kwenye Mikono Ya Milele*, kwenye vipandio vya Ikulu. Saa yenye giza kuliko zote, ndipo Yesu akaja.

116 Ilikuwa ni saa yenye giza kuliko zote aliyोजना Ibrahimu, alipokuwa na umri wa miaka mia moja, ndipo Yesu akaja.

117 Usiku mmoja baada ya kuhubiri kwa muda mrefu, aliwaaga wanafunzi Wake. Nao wakapanda merikebu wakaenda bila Yeye. Na ilionekana, kana kwamba, alipofanya hivyo, basi yuko nje baharini, ile meli ndogo ilikuwa baharini. Ndipo dhoruba ndogo ikatokea. Naye ibilisi akasema, “Nimewapata mbali na Yeye sasa. Nimewapata watakatifu hawa wanaojifingirisha mbali na Bwana wao. Nitaona ni kiasi gani cha Ujumbe watakachopeleka kote ulimwenguni. Nitamzamisha kila mmoja wao huku nje.”

118 Kwa hiyo, kukatokea dhoruba kubwa. Ibilisi akaanza kuvuta pumzi yake, ndipo dhoruba ikatokea. Nayo ile meli ndogo ikaanza kuyumbayumba, namna *hii*. Matanga yakakatika. Makasia yakakatika. Meli ikajaa maji. Na ilikuwa ni wakati wa giza kuliko zote. Bila shaka walikuwa wameshikana kiunoni, huku wakilia. Waliwazia, “Loo, ameenda wapi? Amepatwa na nini? Kwa nini hatukungoja na kumchukua aende pamoja nasi? Kwa nini hatukuwa Naye kwenye mashua?”

119 Na mara nyingi, unaweza kufikiria jambo lile lile. Rafiki yangu, huenda ulikwenda bila Yeye, lakini, kumbuka, Yeye

angali anakutazama. Anajua pale ulipo. Wanaweza kuwa na shida nyumbani kwako. Kunaweza kuwa na shida nafsiini mwako. Kunaweza kuwa na shida mwilini mwako. Chochote kile, usijali. Ameweka macho Yake kwako. Anakutazama.

<sup>120</sup> Alipanda juu ya mlima. Alikuwa akiangalia huko nje, Naye akaona kila mbinu ambayo ibilisi alikuwa akicheza. Haleluya!

<sup>121</sup> Hakupanda tu, bali alipanda ngome za Kalvari; sio tu kwenda Kalvari, bali ngome za Utukufuni. Naye ameketi usiku wa leo, kwenye Ukuu. Anatazama chini duniani. Hakuna hata ki—kiwimbi kinachoweza kuja juu ya maji pasipo (Yeye) ni kwa idhini Yake; bahari haiwezi kusogea; jani haliwezi kusogea; ndege hawezi kuruka. Loo, Jina la Bwana libarikiwe!

<sup>122</sup> Yeye yuko juu ya falme zote na mamlaka yote. Dunia ilimfanyia jina duni kuliko yote liwezalo kuletwa; Mungu akampa jina kuu zaidi ambalo lingeweza kutolewa. Dunia ilimshusha chini kadiri walivyoweza kumfikisha, katika kaburi la dhambi; lakini Mungu akamwinua Juu kabisa. Yeye yuko juu sana hata inambidi kutazama chini apate kuona Mbingu.

Jicho lake liko juu ya shorewanda,  
Na ninajua Yeye ananiangalia.

<sup>123</sup> Anakutazama. Anajua kila wazo lililo akilini mwako. Anajua kila kitendo unachofanya. Anajua kila kitu kukuhusu. Hiyo ni kweli.

<sup>124</sup> Unasema, “Lakini, nimerudi nyuma, Ndugu Branham.” Hiyo haileti tofauti hata kidogo. Yeye anajua sababu hasa ya wewe kurudi nyuma. Anajua ulipo hasa.

<sup>125</sup> Unasema, “Vema, Ndugu Branham, nilienda bila Yeye, pia. Nilikuwa na fursa, wakati mmoja, ya kuzungumza. Nilikuwa na fursa, wakati mmoja, ya—ya kuwa Mkristo. Nilikuwa na fursa. Mhubiri alitoa wito, nami nilipaswa kwenda. Nilijaribu mara moja, lakini nikashindwa. Nilifanya *hiki, kile*.” Haijalishi umefanya nini, bado anakutazama.

<sup>126</sup> Hao wanafunzi walikwenda bila Yeye. Na ile saa yenye giza zaidi, wakati huyo ibilisi alipowaondoa pale, mbali na Uwepo Wake, akaanza kuwashambulia.

<sup>127</sup> Labda ndivyo anavyokufanyia usiku wa leo. Anaweza kukupa kansa. Anaweza kukupa *huu*. Anaweza kukupa *ule*. Anaweza kukupa nyumba iliyovunjika. Anaweza kukupa moyo uliovunjika. Anaweza kukupa wasiwasi. Anaweza kukupa maumivu ya kichwa. Sijui atafanya nini. Lakini kuna jambo moja ninalojua, kwamba Mungu angali anakutazama. Hii inaweza kuwa ndiyo saa yako yenye giza kuliko zote. Sijui; Mungu anajua.

<sup>128</sup> Lakini katika saa hiyo yenye giza kuliko zote, walipokuwa karibu tu kuzama, ndipo Yesu akaja akitembea, kutoka majini,



bila wasiwasi hata kidogo. Hayo mawimbi makubwa yalishuka tu mbele Zake, alipokuwa akitembea.

Petro akasema, “Bwana, ikiwa ni Wewe, niamuru nije Kwako.”

Akasema, “Hima. Njoo huku.”

<sup>129</sup> “Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtapata; bisheni nanyi mtafunguliwa. Kwa maana kila abishaye atafunguliwa; kila atafutaye atapata.” Hakika. Bado anatazama. Na jambo la kushangaza juu yake, wakati hao wanafunzi walipokuwa hawajiwezi na hawana matumaini, na wakati Yesu alipowajia, ndicho kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia, nao walimwogopa. Walimwogopa sana.

<sup>130</sup> Nami ninasema leo, rafiki, kwamba wakati mataifa yameshindwa, kwamba wakati watu wameshindwa, wakati jamii zimeshindwa, ambapo kanisa limeshindwa, ambapo kila kitu kingine kimeshindwa, inaonekana kana kwamba tumekwisha kabisa. Na wakati wowote, saa yoyote, unaweza kusikia sauti, wala hungeweza kumaliza mayowe hayo mpaka ulimwengu wote utakapoangamizwa. Mrusho mmoja wa mabomu ungefanya hivyo. Hayo ndiyo yote unayopaswa kufanya, mmoja tu. Sio lazima waondoke Moscow. Wanaweza kuketi pale pale na kurusha moja kwenye Barabara ya Nne, huko Louisville. Nasi tunaweza kusimama papa hapa na kurusha moja huko Moscow, pia.

<sup>131</sup> Na itakuwaje wakati meli hizi kubwa zimewekwa baharini namna hii, huku roketi zimeelekezwa moja kwa moja kwenye miji hiyo? Moja upande huu, imelenga *huku*; na moja upande huu, imelenga *huko*. Ya kwanza kurushwa, hizi zitarushwa huko.

<sup>132</sup> Itakuwaje? Nyumba yako itakufaa nini wakati huo? Pesa zako zitakusaidia nini basi? Rafiki yako wa kiume atakufaa nini, au rafiki yako wa kike atakufaa nini? Kitu chochote kitakufaa nini? Kama huko sawa na Mungu, umepotea, kwa wakati na Umilele.

<sup>133</sup> Hii ndiyo saa ya giza kuliko zote ambayo ulimwengu huu umewahi kukabili tangu mwanzo wa wakati. Hakuwapata kuwa na wakati katika historia yote ya ulimwengu ambapo ni giza kama ilivyo hivi sasa.

<sup>134</sup> Kansa inavuma. Hebu fikiria, kwamba... Nilisikia taarifa hivi majuzi, mswada kama huu, “Kwamba kutakuwa na watu wengi zaidi watakaokufa Marekani mwaka huu, kutokana na kuvuta sigara, kusababisha kansa, ambao watakufa mwaka huu Marekani, kuliko waliouawa katika miaka minne ya Vita vya Korea.” Kansa inavuma.

<sup>135</sup> Magonjwa yanatokea, na kila kitu kinafanyika. Vema, hatujui tutarajie nini. Madaktari hawajui wayaite hayo magonjwa nini, kwa hivyo wanasema, “Hivyo ni virusi.”

Virusi ni nini? Muulize daktari. Ni kitu ambacho hajui chochote kukihusu. Anasema tu, “Ni virusi.” Hamna lingine.

<sup>136</sup> Kuna maskini vijidudu vidogo na pepo wanaoruka, ambao mwanadamu hakuwahi kuwasikia hapo awali. Kila kitu kinasonga mbele. Kila kitu, tunajaribu kukizuia kwa vitu vya asili. Lakini, tunapajaribu kufanya hivyo, kitu kingine kinatokea. Hiyo ni kweli. Ukimpa mtu penisilini kwa ajili ya *huu*, itaanzisha kitu kingine. Unampa *hii*, ni . . .

<sup>137</sup> Nyote mmeiacha njia. Mungu anayo njia, tafadhali tuingie ndani yake.

<sup>138</sup> Makanisa yameshindwa. Wapresbiteri wameshindwa. Wamethodisti wanashindwa. Wabaptisti wameshindwa. Wapentekoste wameshindwa. Pilgrim Holiness inashindwa. Church of God imeshindwa. Sisi, kila mmoja, ameshindwa. Hiyo ni kweli. Huwezi kusema, “Mimi ni Mmethodisti,” na kujifanya salama. Huwezi kusema wewe ni Mbaptisti na kujifanya salama; Mmethodisti, ama Mpresbiteri, chochote kile, ama Mpentekoste. Huwezi kusema uko salama, si kuwa wa kanisa, kwa sababu kanisa limeshindwa vibaya sana.

<sup>139</sup> Ugonjwa umeenea sana hata, naamini, watano kati ya wanane, ama kitu kama hicho, watakufa mwaka huu, kutokana na kansa. Wazia hilo. Na magonjwa ya kila namna, magonjwa mapya, na vitu vinatokea, ambavyo ni vibaya sana kuwazia.

<sup>140</sup> Magari yanaua. Na kila siku, watu wanaendesha magari barabarani kwa wasiwasi sana, na kupiga mayowe.

<sup>141</sup> Mbona, nilikuwa nikishuka mtaani huko Louisville, jana, na mwanamke fulani alitaka kunipiga kofi niondoke barabarani. Nilikuwa nikitembea namna *hii*, naye mke wangu alikuwa pamoja nami, ndipo nikasikia mtu fulani nyuma yangu. U—umati ulikuwa ninii tu . . . Na mwanamke fulani anayeonekana mjinga, huku anavuta sigara, akasema, “Vema, sasa, ikiwa hujui ni upande gani wa barabara unataka kutembelea, ondoka barabarani.”

Nikasema, “Vema, mama . . .”

Akasema, “Nyamaza!” Haya basi. Haya basi.

<sup>142</sup> Ni nini? Ni jakamoyo. Ni kurukwa na akili. Nao madaktari wanadai kuwa Wamarekani tisa kati ya kumi wanaugua ugonjwa wa kupungukiwa na akili. Hata madaktari wa magonjwa ya akili, wanaodaiwa kuwa wafasiri wa akili, wanarukwa na akili na kuingia kichaa. Wanawafunga kwa pingu kubwa, katika hospitali ya wendawazimu.

<sup>143</sup> Kichaa kinaongezeka. Ubakaji unaongezeka. Wiski inaongezeka. Dhambi inaongezeka. Uanuwai unaongezeka. Hakuna njia ya kuuzuia. Ukomunisti unaingia kama mafuriko. Hakuna njia ya kuuzuia, kwa sababu wako serikalini na popote pale.

144 Loo, lakini, Mungu atukuzwe! Katika saa hii tu yenye giza kuliko zote, ndipo huyu hapa Yesu anaingia, huku mkono wake umenyoshwa, akionyesha ishara na maajabu, na kuwapa watu wokovu na rehema. Saa yenye giza kuliko zote ulimwengu huu uliyowahi kuona! Wakati, mwamba wa Gibraltar utalipuliwa vipande vipande, siku moja. Lakini, Mwamba wa miaka utasimama milele, kama kumbukumbu ya ufufuo, Kristo.

145 Mungu awabariki enyi watu! Mungu awabariki, watoto! Unaweza kuwa maskini. Huenda usijue mlo unaofuata unatoka wapi. Lakini, kuna jambo moja, umekaribishwa tu kwenye Chemchemi ya Uzima usiku wa leo, kama mtu tajiri kuliko wote ulimwenguni. Unakuja bila pesa, bila gharama. Ni wazi kwa yeyote atakaye.

146 Ni saa ya giza kuliko zote ambayo familia hiyo imewahi kuona. Angalieni familia zikivunjika. Kuna talaka nyingi zaidi Marekani, pekee, kuliko ilivyo katika ulimwengu wote ukiwekwa pamoja. Talaka zinaongezeka sana. Uaminifu na u—unyenyekavu na uanamama wetu wa Marekani umeenda wapi? Waangalie wanaume, na yote wafanyayo ni kuenda kasi barabarani, wakijaribu kugonga kila kitu njiani mwao, wawezacho, wakishuka, na kunywa pombe kabla hawajaenda nyumbani.

147 Waangalie wasichana wetu matineja wakishuka barabarani, sigara mikononi mwao. Na kwa hivyo haijalishi ni kiasi gani sayansi ya matibabu inatoa onyo, “Ni kansa! Ni kansa!” Hawajali. Hawajali. Watazipulizia moja kwa moja, kwa vyovyote vile.

148 Mhubiri anaweza kusimama na kuhubiri mchana kutwa, na kuwaambia ni makosa, nao watasema, “Loo, ewe mzee mlokole.” Ulimwengu uko tayari kwa ajili ya hukumu, nasi tutaipokea. Shika neno langu, haitachukua muda mrefu sana kabla jambo fulani halijatukia.

149 Nilipoona uamsho huu, ulioenea katika muda mfupi sana. Ukaenda kule. Nami nikisimama pale, hiyo Nyota ya Asubuhi ilining’inia mtoni, miaka ishirini na kitu iliyopita, aliposema, “Huu Ujumbe utaenea kote ulimwenguni.” Na kumekuwako na kumwagwa kwa Roho Mtakatifu kwa mtindo wa kale wa Kipentekoste, na mioto ya uamsho na uponyaji imeufunika ulimwengu.

150 Walifanya makosa mengi. Gazeti limeandika hapa, si muda mrefu uliopita, katika McCrall, au, la McCall, wakati mtu huyo alipoutishia mkutano wangu kule Minneapolis, baadhi yao, Bw. Peterson na hao wengine, walikuja wakiniambia ya kwamba walikuwa mkutanoni. Nikasema, “Hapana shaka hata kidogo. Lakini hamkuchunguza makala zenu sawasawa. Mlisema A. A. Allen aliandika kitabu hicho. Na A. A. Allen hakuwa na uhusiano wowote nacho. Basi, kama hilo lilikuwa

ni kosa kama hilo, ninaamini mengine yote ni makosa mengi.” Nilisema, “Kweli, hao ndugu wanaweza kustahili kukosolewa sana. Walifanya makosa mengi. Hiyo ni sawa. Lakini, ndugu, ni afadhali nipatikane kwenye uwanja wa vita, nikifanya makosa, kuliko kuwa mkosoaji wa mtu anayejaribu kuwafanya watu waokolewe kwa Mungu.” Unafanya nini kuhusu hilo?

<sup>151</sup> Jina la Bwana Mungu libarikiwe! Nguvu za Bwana Yesu Kristo zinatoshia vivyo hivyo usiku wa leo. Ndizo Mwamba pekee. Ndizo tumaini pekee. Ndizo Imani pekee. Naye Kristo ameziwasilisha kwako.

<sup>152</sup> [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . na kuishi, au kugeuka na kufa. Ni saa ya giza kuliko zote ambayo ulimwengu umepata kuona. Lakini Yesu amekuja, Naye yuko hapa sasa. Baraka Zake ziko wazi. Ubavu wake umechomwa. Mikono yake imenyoshwa. “Na yeyote atakaye, anaweza kuja na kunywa kutoka katika chemchemi za Uzima, bure.” Wewe fanya chaguo lako. Kikomo chako cha Milele kitakuwa—kitategemea msimamo wako kwa Yesu Kristo. Hii inaweza kuwa nafasi yako ya mwisho.

<sup>153</sup> Na tunapoinamisha vichwa vyetu sasa kwa ajili ya maombi, nitamwomba dada aje kwenye piano.

<sup>154</sup> Na wakati kila mtu akiwa katika maombi, ninawatakeni mliwazie tena. Ungeweza kwenda wapi usiku wa leo? Ni nini kingetokea usiku wa leo ikiwa mshtuko wa moyo ungekupata? Hii inaweza kuwa ndiyo nafasi ya mwisho uliyo nayo. Litafakari sasa. Jambo ni kwamba, hivi hutachukua nafasi hii?

<sup>155</sup> Unasema, “Vema, mimi kidogo ni mchanga.” Loo, ndugu, dada, Yeye habagui umri. Unaweza kuvuka mstari ukiwa mdogo au ukiwa mzee; haijalishi. Unaona?

<sup>156</sup> Baba yetu wa Mbinguni, Ujumbe huu tunakupa Wewe sasa, katika Jina la Kristo. Ni saa ya giza kuliko zote ambayo ulimwengu umeona. Ni wakati wa giza kuliko zote ambao historia ya mwanadamu imewahi kuandika. Kuna makombora angani, visahani virukavyo, ndivyo wanavyoviita.

<sup>157</sup> Ulisema, “Kutakuwa na ishara mbinguni; na katika nchi, matetemeko makubwa ya nchi yanayotikisa sehemu mbalimbali, milipuko ya volkeno; mawimbi makubwa baharini.” Ulisema, “Bahari ikivuma. Moyo wa mwanadamu ukishindwa.” Kweli. Ulimwengu haujui la kufanya. Bomu la kwanza la atomiki linalielezea. “Fadhaa ya wakati, dhiki kati ya mataifa.” Ulisema, “Mambo haya yanapotokea, basi inua kichwa chako, Ukombozi wako unakaribia.”

<sup>158</sup> Ninapowazia kule ng’ambo, wale Wayahudi. Ninaona ile nyota ya kale yenye ncha sita ya Daudi, bendera ya kale zaidi ulimwenguni, ikining’inia kule. Kwa nini mataifa hayaioni? Na kuwazia, kwamba taifa letu tunalolipenda litaungana na Waarabu, inaonekana. Watalaaniwa, kwa hakika tu. Wamekataa re—reheema ya Mungu, sasa hawana budi kuistahimili hukumu.

Ona hiyo bendera ya zamani inayoning'inia kule! Tazama jangwa likitoka kama waridi linalochanua! Ona hao Wayahudi wakirudi kutoka huko chini kabisa Irani, wamekuwa kule kwa miaka elfu mbili na mia tano! Biblia ilisema wangechukuliwa kurudishwa Yerusalemu kwa bawa la tai. Kuwaona wale wakuu wa United Airlines wakiwarudisha kwenye mbawa za tai, kama ilivyokuwa. Wakishuka merikebuni, na kutazama, na kusema, "Masihi yuko wapi?"

<sup>159</sup> Ulisema, "Wakati mtini ukitoa machipukizi yake, fahamuni majira ya kiangazi yamekaribia." Tunaona anachipusha. Na tunaona miti mingine yote ikichipusha. Tunajua iko karibu. Tunawaona Ishmaeli na Isaka, kule langoni, wakigombana vikali, kama tu ulivyosema Wewe. Kila unabii sasa hivi unavutia sana. Mungu, wahurumie na uwaokoe waliopotea.

<sup>160</sup> Kama kunaweza kuwa na mmoja hapa usiku wa leo, Bwana, anayekuhitaji Wewe, nena na moyo wake sasa hivi, kwa maana inaweza kuwa ni saa ya giza zaidi. Ingawa huenda tusiitambue. Kunaweza kuwa na baadhi hapa ambao hawatambui kwamba hii ni saa ya giza zaidi, lakini ndivyo ilivyo. Shetani anaweza kuwazamisha katika mambo ya ulimwengu, mpaka hawalitambui.

<sup>161</sup> Ulisema, katika Biblia, "Wewe ni uchi, mnyonge, mwenye mashaka, kipofu, wala hujui."

<sup>162</sup> Mungu, jalia, usiku wa leo, kwamba wanaume kwa wanawake, wavulana kwa wasichana, waweze kujitambua na kutambua kwamba hii ndiyo saa ya giza zaidi ambayo ulimwengu umewahi kuona. Sasa jalia, Bwana, kwamba kama kuna yeyote hapa ambaye hakujui Wewe, kwamba watakuja msalabani kwa utamu na unyenyekevu, usiku wa leo, na kumkubali Kristo kama Mwokozi binafsi.

<sup>163</sup> Je, kuna msimamo kama huo, huku tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu, kwamba ungependa ukumbukwe katika maombi tunapofunga ibada? Naomba uinue mkono wako kwa Mungu, na kusema, "Nikumbuke."

<sup>164</sup> Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, na wewe, na wewe, na wewe. Mungu akubariki huko nyuma. Na wewe, mama, naam. Je, kunaweza kuwa na mwingine kabla tu ya kufunga? Mungu akubariki, ewe msichana.

<sup>165</sup> Unasema, "Ndugu Branham, je, hiyo inamaanisha lolote ninapoinua mkono wangu?" Inategemea tu ulichomaanisha.

<sup>166</sup> Je, unajua, unapoinua mkono wako, unapinga kila kanuni ya sayansi? Je, unajua mkono wako unatakiwa kuning'inia chini, nguvu za uvutano zinaushikilia chini? Unajua, unapoinua mkono wako juu, ya kwamba inaonyesha ya kwamba kuna kitu cha kimbinguni, ndani yako, kimefanya uamuzi? Kitu ambacho si cha asili. Kitu ambacho si cha kisayansi. Ni roho iliyo ndani yako, imekufanya uvunje nguvu za uvutano, kwa

Kiumbe cha kimbinguni kilicho ndani yako, kumwinulia Mungu wa Mbinguni mkono wako na kusema, “Sasa ninamkubali Yesu kama Mwokozi wangu.” Je, unajua ni roho ndani yako inayofanya hivyo? Huwezi kulifanya mwenyewe. Hiyo ndiyo maana yake, tofauti kati ya Uzima na mauti.

<sup>167</sup> Kama umekosea, mwinulie Yeye mkono wako. Kama Yeye humtazama shorewanda anakuona wewe. Hakika.

<sup>168</sup> Sasa, wakati ukiwa papo hapo kwenye kiti chako. Kama unataka kuja madhabahuni na kuomba, hiyo ni juu yako. Ukitaka kubaki kitini mwako, tutakuombea. Unaweza kufanya chaguo lako unataka kuomba kwa njia gani. Mungu atasikia. Kuna yapata mikono dazani moja imeinuliwa.

<sup>169</sup> Sasa, kama unatamani, na unataka Mungu akutendee, pale pale ambapo amekupa imani, mahali papo hapo, Yeye atakuondolea imani. Atajitwika Mwenyewe hukumu yako. Na tayari amelipia.

<sup>170</sup> Naye atasema, “Baba, weka hesabu yake yote Kwangu. Imelipiwa.” Mungu basi atakupa Roho Mtakatifu, papo hapo ulipo.

<sup>171</sup> Kweli ulimaanisha ulipoinua mkono wako? Ikiwa ulilimaanisha, sasa na tuombe.

<sup>172</sup> Mwokozi mbarikiwa, sijui tu ni usiku gani utakuwa mahubiri yangu ya mwisho. Ninataka kuhubiri kila mmoja kama tu ulikuwa wangu wa mwisho. Kwa maana sijui ni lini utakaposema, “Yote yamekwisha sasa. Njoo Nyumbani.” Ninaomba ya kwamba unihifadhi. Ninataka kubaki, kuhubiri Neno. Ninaona haja ya Injili, na kazi inayofanya juu ya wanadamu. Lakini hapa katika nchi yetu nzuri ya Marekani, tumeona urahisi mwingi, utajiri, pesa, kila kitu.

<sup>173</sup> Loo, kamwe hatuwezi kuendelea hivi, huku karibu ulimwengu wote ukifa kwa njaa. Tumelishwa vizuri na kuvikwa nguo, na tunamiliki makazi yetu, magari yetu. Hatuna haja ya chochote, wala hatujui kuwa tu “maskini, wanyonge, vipofu,” tukinena kiroho, “uchi,” bila Damu ya Bwana Yesu. Ingawa, tunaweza kuwa na washiriki wengi kanisani. Tunaweza kuwa na hadhi kubwa ya kijamii katika ujirani. Tunaweza kuvaa vizuri zaidi, kula vizuri zaidi. Lakini, Ee Mungu, kuhusu nafsi hiyo!

<sup>174</sup> Sasa, katika saa hii yenye giza, Wewe ungali hapa, kwa maana unaweka imani juu ya mioyo. Kumekuwa na mikono kadhaa, nadhani, dazani; ninaweza kuwa nimekosea. Huenda ikawa zaidi au kidogo. Mimi sijui, Bwana, lakini Wewe wajua kila mmoja wao.

<sup>175</sup> Na sasa, kwa uchaji, katika maombi ya kumalizia, ninawaleta kwa utamu na unyenyekevu miguuni Pako, kama sifa za mahubiri yangu usiku wa leo, kama tunda la

Ujumbe. Ninawaleta Kwako, Bwana, wanapoinua mkono wao ili niwakumbuke katika maombi. Na wanapiga magoti sasa mioyoni mwao, msalabani. Wapokee, Baba. Wachukue kama watoto Wako wapendwa. Na popote waendapo kanisani, popote pale, loo, jalia wawe mashujaa wa maombi. Jalia wawe waokoaji wa nafsi; wafanye kazi, kwa maana usiku unakuja. Tujalie, Baba. Wachukue katika uangalizi Wako, na uwabariki na uwape shauku kuu ya mioyo yao. Na Roho Mtakatifu mbarikiwa ajaze maisha yao. Kwa maana tunaomba katika Jina la Kristo. Amina.

<sup>176</sup> Ni wangapi wanaompenda Bwana Yesu kwa moyo wao wote? Loo, Yeye si ni wa ajabu? Je, ni wangapi wanaohisi wamesuguliwa kabisa? Ni kama vile tu Bwana alikuwa ameshuka tu na kuchukua brashi Yake kuu ya kusugua na kusugua tu kabisa. Loo, jamani!

<sup>177</sup> Tupe sauti ya huo wa kale, naamini, wimbo wa Jeshi la Wokovu, “Ni nini kinachoweza kuosha dhambi zote? Hakuna ila . . .” [Kusanyiko linasema, “Damu ya Yesu.”—Mh.] “Ni nini kinachoweza kunifanya mzima tena? Hakuna ila . . . [“Damu ya Yesu.”] Hiyo ni kweli. Hebu tuuimbe, sote pamoja, sasa.

Ni nini kinachoweza kuosha dhambi zetu?  
Hakuna ila Damu yake Yesu;  
Nini kinachoweza kunifanya mzima tena?  
Hakuna ila Damu yake Yesu.

Loo, mtiririko ni wa thamani,  
Unaonifanya mweupe kama theluji;  
Sijui chemchemi nyingine,  
Hakuna ila Damu yake Yesu.

<sup>178</sup> Je, huo si ni mzuri sana? Mnazipenda hizo nyimbo za kale? Loo, jamani! Nilitaka kuona kitu sasa. Ni yupi kati yenu . . . Wamethodisti wote inueni mikono yenu. Sawa. Wabaptisti wote inueni mikono yenu. Je, kuna Pilgrim Holiness? Inua mkono wako. Mnazarayo? Inua mkono wako. Church of God? Inua mkono wako. Presbiteri? Inua mkono wako. Je, kuna weza kuwa na Mkatoliki? Inua mkono wako. Angalieni tu makanisa mbalimbali hapa ndani!

<sup>179</sup> Sasa tunapouimba huo tena, ni nini kinachofanya Mpresbiteri mzima? Hakuna ila Damu yake Yesu. Ni nini kinachomfanya Mmethodisti mzima? Hakuna ila Damu yake Yesu. Ni nini kinachomfanya Mnazarayo kuwa mzima? Hakuna ila Damu yake Yesu.

<sup>180</sup> Nini hufanya . . .? Wapentekoste wangapi? Nilisahau kuuliza hilo. Ni Wapentekoste wangapi hapa ndani? Inua mkono wako. Sasa watu wanaona. Wanasema kwamba sisi ni kanisa la Kipentekoste. Kulikuwa na mikono mitano iliyoinuliwa, kwa ajili ya Wapentekoste. Haya basi.

181 Sisi si Wapentekoste, katika madhehebu. Sisi ni Kanisa la Mungu aliye hai. Sisi ni watoto wa Mungu tu. Sisi ni Wapresbiteri. Sisi ni Wamethodisti. Sisi ni Wabaptisti. Sisi ni Walutheri. Sisi ni Wanazarayo. Sisi ni Wapentekoste. Sisi ni Pilgrim Holiness. Sisi ni hao wote. Kwa maana sisi sote tu wamoja, katika Kristo Yesu. Ni nini kilichosababisha hilo? *Hili!*

Ni nini kinachoweza kuosha dhambi zangu?  
Hakuna ila Damu yake Yesu;  
Loo, ni nini kinachoweza kunifanya mzima  
tena?  
Hakuna ila Damu yake Yesu.

Loo, huo mtiririko ni wa thamani,  
Unaonifanya mweupe kama theluji;  
Sijui chemchemi nyingine,  
Hakuna ila Damu yake Yesu.

182 Yeye si ni wa ajabu? Naam, bwana! Sasa tunapoimba, *Chini Msalabani*, nataka Methodisti, na Baptisti, na Presbiteri, na Wapentekoste, na Wanazarayo, wote kupeana mikono, vema, tunapouimba.

Chini pale msalabani . . .

Geuka moja kwa moja sasa, peana mikono na mtu fulani.

Chini ambapo kwa utakaso . . .  
Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;  
Utukufu kwa Jina Lake! (. . . ? . . .)  
Utukufu kwa Jina Lake la thamani!  
Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;  
Utukufu kwa Jina Lake!

183 Sasa huu ni usiku wa ushirika, kama kila mtu ajuavyo. Tunakula ushirika usiku wa leo. Nami nilisahau hilo mpaka Ndugu Neville aliponikumbusha tu.

184 Sasa ni wangapi wanaojisikia vizuri sana, ya kwamba wewe ni Mnazarayo Pilgrim Holiness Pentekoste Baptisti? Hebu tuone mkono wako. Nilikuwa nikiona hapa, Mbaptisti na Mmethodisti wamesimama jukwaani, wakipeana mikono. Loo, hivi sisi. . . Je, si ni ajabu kuwa mtumishi wa Bwana!


185 Sasa sisi ni watoto tu. Nao watoto wana njia za kuchekeza sana, mnajua. Watakuwa wakizozana dakika moja na kucheza kwenye hiyo nyingine. Na hivyo ndivyo tunavyopaswa kuwa. Ondoa tu ugomvi, begani mwako, na uende nje ukajifurahishe zaidi, ukacheze na wanasesere wako, na chochote kinachopaswa kufanywa.

186 Sasa tuna uamsho unaokuja. Nasi tutaimba Injili, tuhubiri Injili, na kuwa tu na wakati mzuri sana. Ni wangapi watakuwa wakiuombea? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Loo, hilo ni zuri. Sasa, njoo utusaidie. Shika simu. Pata kila njia uwezayo,



waalike watoto wote ndani. Waambie, “Njoni huku sasa, na mtusaidie sasa. Tutakuwa na ushirika kwenye Neno.”

<sup>187</sup> Sasa ni wakati wa ushirika. Kila mtu amekaribishwa kula ushirika pamoja nasi, kwa dakika chache tu. Wanauleta hapa madhabahuni, na, dakika kumi ama kumi na tano, yote yamekwisha, kisha tunatawadha miguu.

<sup>188</sup> Ndugu Neville sasa atasoma Maandiko kuhusu ushirika, huku tukiwa na uchaji sana sasa, tunapokula ushirika. 

57-0407E Ndipo Yesu Akaja  
Branham Tabernacle  
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)